**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**


Shule Ya Sekondari Runzewe
S.L.P 55,
**BUKOMBE**
TAREHE 01/06/2023

NAMBA ZA SIMU:
MKUU WA SHULE: +**255755925011/0782534488**
MAKAMU MKUU WA SHULE: **+255763035171/0786581340**
PATRON: +**255757675345.**
***Email***. info@runzewesec.sc.tz
***Websit***e: www.runzewesec.sc.tz


Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………………..
S.L.P……………………………………………………………………
………………………………………………………………………......

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUNZEWE - HALMASHAURI YA BUKOMBE MKOA WA GEITA MWAKA 2023.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2023 tahasusi ya PCB/HGL/HKL. Shule ya Sekondari Runzewe ipo umbali wa kilimita 50 Magharibi ya mji wa Ushirombo. Usafiri wa basi kutoka mjini Ushirombo unapatikana katika kituo cha mabasi Ushirombo. Pia unaweza kufika katika mji wa Runzewe moja kwa moja kutoka sehemu yoyote ya Tanzania.
   Muhula wa masomo unaanza tarehe 03.07.2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13.08.2023 mwisho wa kuripoti ni tarehe 30.08.2023.

2. **Mambo muhimu ya Kuzingatia:**
   2.1 Sare ya Shule.
   a) Sare ya Shule hii ni suruali mbili (2) za rangi nyeusi isiyo na michilizi yoyote na yenye mifuko miwili (2) pembeni na nyuma mmoja (1) isiwe "Modal style" (**Upana miguuni inchi 18+, yenye malinda na**

**lazima iwe na Turn up**) Mashati mawili (2) meupe tetroni Yenye mikono mirefu.

b) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
c) Soksi jozi mbili (2) rangi nyeusi.
d) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
e) Sare ya michezo ni raba, bukta, Tsheti au jezi. (Rangi ya bluu)
f) Nguo za kushindia (Shamba dress) ni mashati mawili (2) ya rangi ya damu ya mzee, mashati hayo yawe ya mikono mifupi na yasiwe na urembo/mapambo au kudariziwa na Suruali nyeusi iliyoelezwa kwenye kipengele (a).
g) Tracksuit moja (1) ya rangi ya bluu.
h) Sweta moja (1) la rangi ya kijani jeshi lenye mstari mweupe kifuani.
i) Tai ndefu ya rangi ya damu ya mzee.
j) Tsheti moja (1) ya rangi ya bluu yenye kola nyeupe.

**ANGALIZO:**

Nguo tofauti na hizo zilizotajwa hapo juu hazitakiwi kabisa shuleni. Sare zilizopo katika kipengele (h) - (j) unaweza kuzipata sehemu yoyote au shuleni kwa gharama zifuatazo:

i. Sweta Tshs. 15,000/=
ii. Tsheti Tshs. 12,000/=
iii. Tai Tshs. 2,000/=
iv. Nembo ya Shule Tshs. 3,000/=

**NB: Michango hii ilipwe shuleni siyo benki.**

2.2 **A. Michango ya shule**;- **JUMLA TSHS 80,000/=**.

Fedha hii ya michango ilipwe kwenye akaunti Na. **32506600010** jina la akaunti Runzewe Secondary School Revenue Collection Benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

**B. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**:

i. Faili moja (folder file)
ii. Jembe lenye mpini, kwanja, reki ya chuma moja (1) ndoo ya lita 20.
iii. Moper moja (01), hardbloom moja (01), softbloom moja (01).
iv. Ream ya karatasi **AA4 (Double 'A') mbili (02) kwa mwaka, Angalau moja(01) kwa kila muhula.**

v. Godoro futi $2\frac{1}{2}$ x 6 na chandarua.
vi. Mashuka pair 2 ya rangi ya pink na blanketi la rangi yoyote.
vii. Sanduku imara la chuma lenye kufuli.
viii. Scientific calculator kwa wanafunzi wa mchepuo wa PCB.
ix. Sahani, bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula.
x. Ndoo moja (ya lita 20) kwa ajili kutunzia maji na usafi binafsi.
xi. Beseni au dishi kwa ajili ya kuogea na usafi.
xii. Vifaa vingine vya kutosha vinavyokubalika shuleni kwa matumizi binafsi kwa muhula mzima. Mfano: sabuni, madaftari, vitabu vya masomo husika n.k
xiii. Picha. (Passport size) 4, 2 za wazazi/walezi na 2 za ndugu wa karibu na mwanafunzi watakaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
xiv. Aje na vitabu binafsi kulingana na tahasusi yake.
xv. Wanafunzi wa Tahasusi ya **PCB** wanaombwa kuja na Laboratory Coat.

***NB:*** **Shule inawashauri wazazi wote kuwakatia Bima ya Afya (NHIF) watoto wao na aje nayo shuleni wakati wa kuripoti.**

**ANGALIZO.**

Fomu zifuatazo zinatakiwa kurudishwa shuleni zikiwa zimejazwa, vizuri,

i. Fomu maalamu kwa wanafunzi.
ii. Fomu ya kiapo cha kutomiliki simu shuleni.
iii. Fomu ya vipimo vya mwnafunzi (vipimo vithibitishwe na Daktari wa Hospitali ya Serikali).

## C. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vii. Kufuga ndevu.
viii. Ulevi na unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xv. Kumiliki, kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xvi. Kudharau bendera ya taifa
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xviii. Uharibufu wa mali za Umma kwa makusudi.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

R.B.HALILI
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI RUNZEWE
S.L.P. 55
BUKOMBE - GEITA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE.

## SHULE YA SEKONDARI RUNZEWE

### .S.L.P 55 – BUKOMBE-GEITA.

# MEDICAL EXAMINATION FORM

**PART A:** TO THE MEDICAL OFFICER.

Name of student…………………………………………………..

Kindly, examine the abave named student as to his/her physical and mental fitness for being registered into full time ordinary secondary studies.

| S/N | EXAMINATION CONDITIONS | STATUS/ REMARKS |
|---|---|---|
| 1 | **Physical abnormality** | |
| 2 | **Hearing ability** | |
| 3 | **Urine** | |
| 4 | **Stool** | |
| 5 | **Tuberculosis** | |
| 6 | **Psychosis** | |
| 7 | **Epilepsy** | |
| 8 | **Sight** | |
| 9 | **Blood pressure** | |
| 10 | **Speech** | |
| 11 | **Pregnance** | |

Any other health problem________________________________________________

________________________________________________________________

**PART B:** (To be completed by the Government medical officer)

I have examined the condition of the student and consider that he/she is **FIT/ UNFIT** to pursue this level of studies.

DATE…………………………………….. SIGNATURE…………………………………

STATION……………………………………DESIGNATION…………………………..

**4. KUHUSU MWANAFUNZI KUMILIKI SIMU SHULENI.**


Kikao cha bodi ya shule cha tarehe 17.08.2017 kilikubaliana na adhabu zifuatazo kwa mwanafunzi atakae kamatwa na simu shuleni:-

1. Kuchapwa viboko vinne 4 mbele ya wanafunzi wate mstarini.
2. Kusimamishwa masomo siku 21
3. Siku ya kurudi shuleni mwanafunzi atatakiwa kuja na mzazi /mlezi wake na faini ya shilingi laki mbili(TSH. 200000).
4. Simu na kadi ya simu vitavunjwa mbele ya wanafunzi na mzazi/mlezi.

N.B Endapo mzazi/mlezi atashindwa kutekeleza vipengele tajwa (i-iv) mwanafunzi atafukuzwa shule.

JINA LA MWANAFUNZI______________________________SAHIHI__________

TAREHE______________________________



# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

## SHULE YA SEKONDARI RUNZEWE

## S.L.P 55 BUKOMBE – GEITA

**FOMU MAALUMU KWA MWANAFUNZI**

1. **MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI:**

(i) Jina la Mwanafunzi ______________________ Jinsia ______ Tarehe ya kuzaliwa ____________

(ii) Shule ya Msingi/Sekondari aliyotoka ______________________

(iii) Jina la Baba ______________________ Kazi yake ______________ Na. ya simu ____________

(iv) Jina la Mama ______________________ Kazi yake ______________ Na. ya simu ____________

(v) Kijiji/Mtaa wanapoishi ______________ Wilaya ______________ Mkoa ____________

(vi) Dini ______________________

(vii) Majina ya ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kutoa msaada pindi wanapohitajika:

a) ______________ anakoishi ______________ Na. ya simu ____________

b) ______________ anakoishi ______________ Na. ya simu ____________

c) ______________ anakoishi ______________ Na. ya simu ____________

d) ______________ anakoishi ______________ Na. ya simu ____________

(viii) Michezo anayoweza kushiriki mwanafunzi shuleni:

______________ ______________ ______________

NB: Je wazazi wote wako hai? *Ndiyo/Hapana (*Kata isiyositahili)

Kama amefariki/wamefariki, aliyefariki ni ______________________

2. **KUKUBALI NA KUTII SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE:**

Mimi (Jina la Mwanafunzi) ______________________ naahidi sitashiriki kabisa katika fujo/migomo na kutenda makosa ya jinai shuleni na maeneo mengine. Pia, naahidi kuzifuata taratibu na sheria zote za shule kwa faida yangu binafsi, shule na Taifa kwa ujumla. Endapo nitakwenda kinyume na taratibu na kanuni za shule nakubali kufukuzwa shule, kusimamishwa masomo na kufikishwa mahakamani au kupewa adhabu nyingine kulingana na sheria.

JINA LA MWANAFUNZI ______________________ SAHIHI ______________ TAREHE ____________

JINA LA MZAZI/MLEZI ______________________ SAHIHI ______________ TAREHE ____________

3. **MZAZI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA, MICHANGO NA KUTEKELEZA MAELEKEZO YA SHULE:**

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi) ______________________ nakubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada na michango yote kwa wakati mwafaka na kutekeleza maelekezo yatolewayo na shule.

Vilevile, naahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa uongozi wa shule pindi nikihitajika kuhusu tabia, mwenendo au suala jingine lolote linalomhusu mtoto wangu.

JINA LA MZAZI/MLEZI ______________________ SAHIHI ______________ TAREHE ____________

______________________

MKUU WA SHULE

FOR HEADMASTER
RUNZEWE SEC. SCHOOL
P.O. BOX 55
BUKOMBE - GEITA